OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

SHULE YA SEKONDARI MADILU

S.L.P 787,NJOMBE.

TAR……..

Kumb. Na…….

JINA LA MWANAFUNZI: …….

S.L.P……

SHULE YA MSINGI……..

LUDEWA.

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MADILU, WILAYA YA LUDEWA MKOA WA NJOMBE, MWAKA……</u>

1.0.UTANGULIZI

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Madilu iliyopo umbali wa Km 2 kusini mwa ofisi ya kata Madilu/Kijiweni kupitia Zahanati ya kijiji cha Madilu. Usafiri wa pikipiki/maarufu kwa jina la bodaboda unapatikana kutoka ofisi ya kata Madilu/kijiweni mpaka shuleni kwa Tshs. 1000/= tu. Mhula wa kuanza masomo unaanza tarehe…… unatakiwa kuripoti shuleni tarehe…….. Na mwisho wa kuripoti ni tarehe……. Ndani ya siku saba usiporipoti hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi/mlezi kulingana na agizo la serikali na kama mwanafunzi/mototo umempeleka shule binafsi basi ulete barua ya uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa shule aliko ripoti mwanafunzi.

2.0.**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**.

2.1. SARE ZA SHULE.

a) Sare za shule ni suruali za kijani mbili na shati nyeupe mbili za mikono mirefu kwa wavulana na sketi mbili fupi zinazoishia juu ya goti za rangi ya kijani, suruali mbili za kijani na shati mbili nyeupe za mikono mifupi kwa wasichana (viambatanisho vya sare vimeambatanishwa na barua hii ya kujiunga na kidato cha kwanza)

b) Vazi la baada ya masomo/vazi la shamba kwa wavulana ni suruali mbili za rangi ya udongo/ugoro na sio jinsi na tisheti mbili za rangi ya kijani na wasichana ni gauni mbili za rangi ya bluu bahari (gauni ndefu inayovuka magoti kiatmbaa kizito)

c) Rangi ya hijab ifanane na shati la shule

d) Viatu vyeusi jozi/pea mbili vya ngozi (leather shoes) visivyo na kisigino kirefu vya kufunga na kamba /gidmu

e) Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana

f) Sweta la rangi ya damu yam zee lisilo maandishi yoyote na lililofumwa lenye umbo la “V”

g) Sare za michezo kwa shule hii ni traki suti mbili za rangi nyeusi kwa wasichana na kwa wavulana ni bukta na T-shirt, raba jozi moja na soksi za michezo.

h) Nguo nyingine za ndani za kutosha ni muhimu sana kama vile sidilia au shumizi, chupi n.k

i) Aje na jembe jipya lenye mpini na fagio aina ya chelewa kwa ajili ya usafi

j) Aje na chombo safi (chenye ujazo walau lita tano) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa

k) Aje na vyombo vya chakula kama sahani, bakuli, kikombe na kijiko

l) Aje na sanduku imara (tranker) la kuhifadhia vitu vyake.

m) Aje nandoo ya lita kumi (10) kwa ajili ya kufuria na kuogea

TANBII

a) Tafadhari jaza fomu ya maelekezo binafsi yahusuyo mwanafunzi

b) Tafadhari kwa wasichan mshono umeambatanishwa pamoja na maagizo ya mwanafunzi

c) Hatuhitaji nguo yoyote ambayo haijatajwa humu hasa za nyumbani zinazotofautiana na wenzake

d) Nguo zote ziwekwe alama (jina la mwanafunzi) kwa kudalizi na chelehani

e) Kwa wanaokojoa waje karatasi ya nailoni kwa ajili ya kuweka juu ya godoro ili kuzuia godoro kuloa

2.2 . Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu (Mathematical set)

2.3. Nauli ya wanafunzi kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro na vifaa vya malazi ni jukumu la mzazi/mlezi hivyo hakikisha mwanafunzi ana mahitaji hayo

3.0. MICHANGO YA CHAKULA

A] Fedha ya chakula ni Tshs 110,000/=[Laki moja na elfu kumi tu] fedha hii unaweza kulipa mara mbili au mara moja kwa ulipaji wa mara mbili utakuwa kama ifuatavyo;

i. Mwezi januari anaporipoti aja na TShs. 60,000/=

ii. Mwezi julai inapofungua mhula wa pili TShs 50,000/=

B] Mchango wa mahindi ni kilogramu 200 kwa mwaka na mzazi/ mlezi unashauriwa kutoa mahindi yote ili kuepusha usumbufu

C] Mchango wa maharagwe ni debe mbili kwa mwaka, waweza lipa mara mbili yaani debe moja mhula wa kwanza mwezi januari na debe moja jingine mhula wa pili mwezi wa Julai

D] Mchango wa mchele ni kilo 20 kwa mwaka, mzazi/mlezi unaweza lipia mara mbili mwezi januari mhula wa kwanza kilo 10 na mhula pili mwezi Julai kilo 10

4.0 MCHANGO WA RIMU (KARATASI YA KUCHAPISHIA MITIHANI)

- Mwanafunzi anatakiwa aje na rimu au bunda la karatasi (ream paper A4) kwa mwaka bunda moja kwa ajili ya kuchapishia mitihani ya mihula na majaribio ya kila wiki, mwezi na karatasi hizi pia atakuwa anapewa wakati wa kufanya mitihani

5.0. MATIBABU NA HUDUMA ZA AFYA

a) Kituo au zahanati kwa ajili ya matibabu kipo njiani kuelekea Madilu sekondari pia shule inatoa huduma ya kwanza kwa wanfunzi

b) Kama motto/mwanafunzi hana bima ya afya, aje na Tshs 5,000/- ili tuwaunganishe watoto sita (06) wapewe bima ya jamii iliyoboreshwa kwa ajili ya matibabu pindi wakiumwa

c) Mwanafunzi anapokuwa na matatizo ya kiafya wakati wa saa za masomo asisite kumwona mwalimu wa zamu au mwalimu wa darasa.

6.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA NA MWANAFUNZI SHULENI

i. Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitari ya serikali

ii. Fomu hii itakabidhiwa na kuwasilishwa kwa Mkuu wa shule mara tu utakaporipoti shuleni

iii. Fomu ya maelekezo binafsi kwa ajili ya maendeleo ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katiak migomo, fujo na makosa ya jinai

iv. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri na kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa an shule

v. Fomu ya kupewa mwanafunzi ni ile ya sharia na kanuni za shule ili azisome na kuzielewa

ZINGATIA: tafadhari soma maelekezo haya au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

7,0, MWISHO.

- Nimatumaini yangu kuwa utatumia nafasi hii vyema ili kupata taaluma bora iliyopangwa sambamba na kuzingatia sharia na kanuni zote ili kufanikisha azima yako.

KARIBU SANA MADILU SEKONDARI.

……

MICHAEL M MWALONGO.

KAIMU MKUU WA SHULE

SIMU: 0756 524 162

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995, aidha; inazingatia miongozo yote inayotolewa an Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimsmizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
3. Kushiriki kwa makini kufanya maanadalio ya jioni (preparation)
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
6. Kutunza usafi wa mwili na mavazi na mazingira ya shule
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

3**.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE**.

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadharika
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba
9. Kutoa Mimba
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. Kuwa na simu ya mkononi au kifaa chochote kinachohusiana na simu

xxxx

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA.

SHULE YA SEKONDARI MADILU

S.L.P 787,NJOMBE.

FOMU YA KUKUBARI NAFASI YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA

SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi……nimesoma na kuelewa masharti yote na sharia za shule; nayakuabari/siyakubari. Kwahiyo ninaipokea/siipokei nafasi hii niliyopewa. Ninaaahidi kuwa niatazingatia masharti na sharia zote za shule na nitakuwa mtiifu mpaka kumaliza kidato cha Nne.

Sahihi ya mwanafunzi……Tarehe……

SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

Mimi ……mzazi/mlezi wa ……..

Ninakubari/sikubari nafasi aliyopewa motto wangu, ninaahidi kumtimizia mahitaji yote ya shule na kushirikiana/kusaidiana na walimu kumlea kielimu na kitabia.

Sahihi ya mzazi/mlezi……Tarehe……

HALMASHAURI NYA WILAYA YA LUDEWA

SHULE YA SEKONDARI MADILU

S.L.P 787, NJOMBE.

MAELEKEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

A: HABARI ZA MWANAFUNZI:

1. Jina la mwanafunzi……..
2. Tarehe ya kuzaliwa……..
3. Mahali alipozaliwa: Wilaya…….. Mkoa……..
4. Dini …… Dhehebu……...

B: HABARI ZA WAZAZI

1. Baba yu hai…….. Ndiyo/Hapana……..
2. Mama yu hai……. Ndiyo/Hapana…….
3. Jina la mzazi/mlezi anayekulea…….
4. Uhusiano wako na mlezi (kama huna baba)……
5. Kazi ya mzazi/mlezi…….
6. Anuani ya mzazi/mlezi…….

   ……. Namba ya simu……...
7. Mahali ambapo mzazi/mlezi anaishi kijiji/Mji…….

   Kata…….. Tarafa…… Wilaya…….. Mkoa……

C: NDUGU WENGINE WA KARIBU:

8. Ndugu……..

   Anuani…… Namba ya simu……Uhusiano na wewe……..

D: UTHIBITISHO WA AFISA MTENDAJI WA KATA AU MWENYEKITI WA KITONGOJI/KIJIJI AMBAKO MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ANAISHI

I. Jina la Kiongozi…….. Cheo……

   Anuani…… sahihi na mhuri……

   Namba ya simu…….

II. Jina la kiongozi……. Cheo…….

   Anuani…… sahihi na mhuri……Namba ya simu……...

Tafadhari jaza fomu hii kwa uangalifu. Futa isiyohusika

LUDEWA DISTRICT COUNCIL

MADILU SECONDARY SCHOOL

P.o.Box 787, NJOMBE.

TO;

THE MEDICAL OFFICER,

……

……

……..

Ref: *REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION*.

Please kindly examine…….. (Name) to determine His/Her physical fitness for pursuing secondary school studies.

……

MICHAEL M MWALONGO

ACTING HEADMASTER.

1. Eyesight…….
2. Hearing…….
3. Speech……..
4. Limbs……..
5. Leprosy……..
6. Epilepsy……
7. Cardiac diseases……..
8. Rheumatism……..
9. Venereal diseases…….
10. Pregnancy (for girls)…….
11. Any other serious diseases……..
12. General comments……

    ……..

    …….

    …….

Signature…….. ……

Date and Official Stamp

NB: Any disease detected should be treated.